SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA YA MJI

SURA 288

# SHERIA NDOGO

------------------
(Imetungwa chini ya Kifungu cha 89)
------------------------------

SHERIA NDOGO YA MIFUGO NA UVUVI YA HALMASHAURI YA MJI WA KASULU YA MWAKA 2020

Jina **1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Mifugo na Uvuvi ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu ya Mwaka 2020.

Tafsiri **2.** Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Kasulu;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kasulu au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"machinjio" maana yake ni eneo lililotengwa kwa shughuli ya uchinjaji mifugo.

Wajibu wa Halmashauri **3.-** Halmashauri itakuwa na wajibu:

(a) kutenga maeneo maalum kwa ajili ya machinjio;
(b) kutoa miongozo ya idadi ya mifugo inayopaswa kufugwa na kila mfugaji;
(c) kutenga maeneo maalum ya kupitisha mifugo kwenda machinjioni au malishoni.

Wajibu wa Mfugaji **4.-** (1) Mfugaji atakuwa na wajibu wa:

(a) kulinda, kuhifadhi mazingira na miundombinu inayowazunguka;
(b) kuhifadhi vyanzo vya maji;
(c) kutofuga wanyama wengi katikati ya eneo la mji kwa ufugaji huria au nusu huria;
(d) kufuga kwa ufugaji wa ndani;
(e) kutoruhusu mifugo kuzurura ovyo mitaani.

(2) Mtu yeyote atakayefuga mbwa atatakiwa kuhakikisha mbwa huyo anapewa chanjo na kufungiwa ndani;

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na hivyo atastahili adhabu ya faini au kutaifishiwa mifugo au kifungo;

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

**5.-** (1) Afisa Mwidhiniwa wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii atakuwa na uwezo wa:

(a) kuingia eneo lolote la ufugaji au uvuvi ndani ya muda wa kazi kwa lengo la kufanya ukaguzi;

(b) kumkamata na kumshitaki mtu yeyote anayefanya uvuvi, uchinjaji, usafirishaji wa mifugo kinyume na Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia Afisa Mwidhiniwa katika Kifungu cha kidogo cha kwanza atakuwa ametenda kosa.

Utambuzi wa mifugo

**6.-** (1) Mifugo yote ndani ya Halmashauri itakuwa na alama maalum itakayobuniwa na Halmashauri ili kuitambua.

(2) Kila mfugo utatakiwa kupigwa chapa katika eneo maalum kama itakavyoelekezwa na Afisa Mwidhiniwa ili kuweza kulinda ubora wa ngozi.

Usafirishaji wa mifugo

**7.-** Mtu yeyote anayesafirisha mifugo atapaswa:

(1) Kuwa na kibali cha kusafirisha mifugo.

(2) Kuzingatia haki za wanyama.

(3) Kuzingatia afya ya wanyama wakati wa kusafirisha kama vile chanjo.

(4) Mifugo inayosafirishwa itatozwa tozo kama ifuatavyo:

(a) usafirishaji ndani ya mkoa mbuzi au kondoo shilingi elfu moja na mia tano na nje ya mkoa shilingi elfu mbili na mia tano kwa kila mnyama;

(b) usafirishaji ndani ya mkoa ngombe, punda, nguruwe ni shilingi elfu moja mia tano na nje ya mkoa shilingi elfu mbili mia tano kwa kila mfugo.

Machinjio

**8.-** (1) Kutakuwa na eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa shughuli za uchinjaji na eneo hilo litajulikana kama machinjio ya wanyama.

(2) Kila mfugo utakao ingia machinjioni utalipiwa ushuru wa machinjio, usafi na gharama za upimaji ambapo n'gombe atalipiwa shilingi elfu mbili na mia tatu na kwa upande wa mbuzi na kondoo watalipiwa shilingi elfu moja na mia tano.

(3) Kila mdau wa machinjio lazima aingie ndani ya machinjio akiwa na sale maalum ya machinjio, koti jeupe na viatu virefu.

(4) Kila mdau wa machinjio lazima apimwe afya yake.

(5) Wadau wote wa machinjio lazima wazingatie usafi na utunzaji wa miundombinu ya machinjio.

(6) Hairuhusiwi mtu yeyote kuanzisha machinjio bila kibali cha Mkurugenzi.

(7) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote asiye mchinjaji au mchunaji kuingia ndani ya machinjio bila ruhusa ya afisa mifugo.

(8) Mtu yeyote atakayechinja mfugo eneo lisiloruhusiwa atakauwa ametenda kosa.

Uuzaji nyama

**9.** Nyama zote ni lazima zikaguliwe na maafisa mifugo au afya kabla ya kuingizwa sokoni kwa matumizi.

Mazao ya Uvuvi

**10.-** (1) Kila mfanyabiashara wa mazao ya uvuvi atapaswa kuwa na leseni ya kukusanya na kuendesha biashara hiyo katika eneo lote la Mji ambayo italipiwa kiasi cha shilingi elfu kumi.

(2) Kila atakaye safirisha mazao ya uvuvi atatakiwa kuwa na kibali cha usafirishaji wa mazao hayo na atapaswa kulipa ushuru wa shilingi elfu mbili kwa kila tenga au gunia.

(3) Hairuhusiwi gari lisilo na kibali kuhamisha mzigo katika gari lenye kibali labda pale itakapothibitika kuwa gari hilo limeharibika.

Makosa na adhabu

**11.** Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

**12.** Bila kujali masharti ya kifungu cha 11, Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi cha shilingi laki mbili endapo mtu huyo atakiri kosa kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii na kulipa kiasi anachodaiwa.

## JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 12)

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………… wa S.L.P. ………………………… nakiri kutenda kosa la …………………………………………………. ikiwa ni kinyume na kifungu cha ……………… cha Sheria ya Ndogo ya Mifugo na Uvuvi ya Halmashauri ya Mji Kasulu ya Mwaka 2020.

Kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa kiasi cha shilingi laki mbili badala ya kushtakiwa Mahakamani iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha……………………………………………………… cha Sheria Ndogo hii.

Saini: ………………………………………………...

Tarehe ……………………………………………………

Mbele yangu: -

Jina: …………………………………………….….

Saini: …………………………………………….….

Wadhifa: ………………………………………………...

Tarehe ……………………………………………………

Nembo ya Halimashauri ya Mji Kasulu imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Kasulu kilichopita tarehe 06 Mwezi FEB, Mwaka 2018.

Nakubali

Dodoma — **SELEMANI S. JAFO (MB)**

16th July,2020 — WN OR - TAMISEMI